

# **JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**



## **WIZARA YA AFYA**

### **TAARIFA KWA UMMA KUHUSU KUENDELEZA TAHDHARI DHIDI YA MAGONJWA YA KUAMBUKIZA IKIWEMO TISHIO LA UGONJWA WA EBOLA**

**KAGERA, 02 Novemba, 2022.**

#### **Ndugu Wananchi,**

Itakumbukwa kuwa tarehe 20 Septemba 2022, tulipokea taarifa ya mlipuko wa ugonjwa wa Ebola katika Wilaya ya Mubende nchini Uganda. Ugonjwa huo umeendelea kusambaa na kufikia Wilaya 10 ikiwemo jiji la Kampala na Entebbe, na hadi kufikia tarehe 31 Oktoba, 2022 jumla ya wagonjwa 130 wamethibitika kuwa na ugonjwa huo na 43 kufariki. Aidha, hivi karibuni kumekuwa na taarifa za mlipuko wa ugonjwa wa Kipindupindu katika nchi jirani na pia katika maeneo machache ya nchi yetu.

#### **Ndugu wananchi,**

Ili kuendelea kuwa salama na kuepuka magonjwa ya mlipuko kama Kipindupindu na Ebola, ninawasihi wananchi wote kuendelea kuzingatia yafuatayo:

- a) Kuendeleza utamaduni wa kunawa mikono mara kwa mara kwa maji tiririka na sabuni au kutumia vitakasa mikono ili kujikinga na magonjwa ya kuambukiza kama kipindupindu, UVIKO 19, Ebola na mengine ambayo yameonekana kuweza kuzuilika endapo jamii itazingatia suala la kunawa mikono.

- b) Kuhakikisha kila mtu anakuwa na vifaa vya kuwezesha usafi wa mikono katika maeneo ya kazi, biashara na majumbani.
- c) Kuepuka kushikana mikono au kugusa majimaji ya mwili wa mtu yejote ikiwemo jasho, mkojo, kinyesi au damu.
- d) Katika kipindi hiki cha tishio la Ebola, unapomwona mtu yoyote aliyepata shida ya kiafya ghafla ni vyema kuchukua tahadhari kwanza kabla ya kuwahi kumshika bila kinga ili kuepuka kupata maambukizi endapo ni ugonjwa hatari wa kuambukiza.
- e) Kuendelea kutoa ushirikiano wa kupimwa dalili za Ebola katika baadhi ya maeneo ya mipaka na viwanja vya ndege.
- f) Endapo mtu yoyote atapata dalili zozote za kiafya, awahi hospitali iliyoko karibu nae au kupiga simu namba 199 kwa msaada wa dharura.
- g) Watalaam katika hospitali zote kuendelea kuchunguza dalili za ugonjwa wa Ebola ili kuubaini mapema na kuhakikisha wanatoa taarifa kwa mamlaka husika pale panapokuwa na mhisiwa.

***Chukua Hatua Mapema, Magonjwa ya Kuambukiza yanazuilika,  
Kinga ni Bora kuliko Tiba!***

Imetolewa na;



Prof. Tumaini J. Nagu

**MGANGA MKUU WA SERIKALI**